

**BENKI KUU YA TANZANIA**

16 Barabara ya Jakaya Kikwete  
S. L. P. 2303  
40184 DODOMA  
TANZANIA  
Simu: +255 22 223 3167  
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz

**BANK OF TANZANIA**

16 Jakaya Kikwete Road  
P.O. Box 2303  
40184 DODOMA  
TANZANIA  
Phone: +255 22 223 3167  
Email: botcommunications@bot.go.tz

**03 Januari 2024****TAARIFA KWA UMMA  
WANAOKOPESHA BILA LESENI KUCHUKULIWA HATUA**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kukumbusha umma kuwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018, ni kosa kwa taasisi, kampuni au mtu binafsi kujihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila ya kuwa na leseni.

Hivyo, Benki Kuu ya Tanzania haitasita kuwachukulia hatua za kisheria, taasisi, kampuni au watu binafsi wanao fanya biashara ya kukopesha bila ya kuwa na leseni. Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 16(2)(a) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, hatua zitakazochukuliwa kwa ukiukaji wa Sheria ni pamoja na faini isiyopungua Shilingi Milioni 20 au kifungo cha muda usiopungua miaka miwili au vyote viwili kwa pamoja.

Benki Kuu inawakumbusha wakopaji wote kuhakikisha wanasoma mikataba ya mikopo inayotolewa na wakopeshaji, kuelewa na kukubaliana na vigezo na masharti ikiwa ni pamoja na riba na gharama nyingine za mikopo hiyo. Tunasisitiza kuwa mkopeshaji anatakiwa kutoa nakala ya mkataba wa mkopo kwa mkopaji, kadhalika mkopaji ana haki ya kudai na kupewa mkataba wa mkopo kila anapochukua mkopo.

Tunapenda kuusisitiza umma kuepuka kukopa au kufanya biashara na taasisi, kampuni au mtu binafsi ambae hana leseni kutoka Benki Kuu. Aidha, orodha ya taasisi, kampuni na watu binafsi wenye leseni za biashara ya kukopesha zinatolewa na Benki Kuu ya Tanzania kwenye tovuti yetu ambayo ni [www.bot.go.tz](http://www.bot.go.tz).

**Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:**

Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha  
Idara ya Usimamizi wa Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha  
Benki Kuu ya Tanzania  
2 Mtaa wa Mirambo, S.L.P 2939 Dar es Salaam  
Simu Na. +255-22-223-5585;  
Barua Pepe: [info@bot.go.tz](mailto:info@bot.go.tz) or [botcommunications@bot.go.tz](mailto:botcommunications@bot.go.tz)

**EMMANUEL M. TUTUBA  
GAVANA  
BENKI KUU YA TANZANIA**